

**Mpinga Kristo**  
**(Antichrist)**

**Na**

**Alex S. Silvester**

**Mpinga Kristo**  
**(Antichrist)**

**Na**

**Alex S. Silvester**

**Oktoba 11, 2018**

# Mpinga Kristo

Nilipokuwa kijana mdogo kabla sijafanyika Mkristo, nimewahi kusikia mambo makubwa kuhusu “Wapinga Kristo.” Kila mmoja kwa wale walioua watu wengi katika siku zao, kama Hitler wa Atilla na Stalin wameshutumiwa kwa kuwa ni “Wapinga Kristo.” Nakumbuka mmoja wa marais wan chi hii alipokuwa madarakani. Na baadhi ya marafiki zangu walishawishika na wakanishawishi pia, kwamba alikuwa “Mpinga Kristo,” kwa sababu alikuwa Muislamu. Na kwamba anaweza kubadilisha mambo kuwa yasiyopaswa kuwa, sote tunaweza kuharibiwa. Nakiri kwamba kila mmoja aliogopa kufa. Kila wakati kukitokea vita Mashariki ya Kati, au sehemu nyingine ya dunia, baadhi wanashutumiwa kwa kuwa “Wapinga Kristo.” Vita ya ghuba ilipoanza, vitabu kadhaa vilihaririwa na wanadini juu ya Ufunuo wa Biblia. Hataivyo, Sadam Husein aliongelewa kama Mpinga Kristo na watu wengi ulimwenguni kote waliogopa. Baada ya kusoma baadhi ya vitabu hivi, “Biblia inafundisha” ingetutaka tuamini kwamba mpinga Kristo alitajwa katika kila ukurasa wa kitabu cha Ufunuo. Ukweli wa mambo ni kwamba neno mpinga Kristo haipatikani hata mara moja katika kitabu cha Ufunuo. Unaweza kusoma mwenyewe na kuona kwamba hii ni kweli. Hakika neno “Mpinga Kristo” inapatikana mara nne tu katika Agano Jipya. Inapatikana mara tatu katika waraka wa kwanza wa Yohana, na mara moja katika waraka wake wa pili. Na huu ndio ukweli ambao Biblia inafundisha kuhusu Mpinga Kristo.” *“Watoto ni wakati wa mwisho na kama vile mlivyosikia kwamba mpinga Kristo yuaja, hata sasa wapinga Kristo wengi wamekwisha kuwako. Kwa sababu hiyo twajua ya kuwa ni wakati wa mwisho. Walitoka kwetu lakini hawakuwa wa kwetu. Maana kama wanalikuwa wa kwetu wanalikaa pamoja nasi. Lakini walitoka ili wafunuliwe kwamba ssi wote walio wa kwetu.”* (Yoh. 2:18-19). Kifungu kinawaongelea wale tulio nao katika kusanyiko lakini sio wa kweli na hawazai matunda. Wapo kwa muda mfupi na baada ya hapo wanatoka. *“Ni nani aliye mwongo ila yeye akanaye ya kuwa Yesu ni Kristo? Huyo ndiye mpinga Kristo, yeye amkanaye Baba na Mwana. Kila amkanaye Mwana, hanaye Baba; amkiriye Mwana anaye Baba pia.”* (1 Yoh. 2:22-23). *“Katika hili mwamjua Roho wa Mungu; kila roho ikiriyo kwamba Yesu kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu. Na kila roho isiyomkiri Yesu haitokani na Mungu. Na hii ndiyo roho ya mpinga Kristo ambayo mmesikia kwamba yaja; na sasa imekwisha kuwako duniani.”* (1 Yoh. 4:2-3). *“Kwa maana wadanganyifu wengi wametokea duniani, waisiokiri ya kuwa Yesu Kristo yuaja katika mwili. Huyo ndiye yule mdanganyifu na mpinga Kristo.”* (1 Yoh. 1:7). Angalia kwamba mpinga Mkristo anatafsiriwa kwamba ni yule anayekataa kwamba Yesu ni Kristo. Hata katika undugu, wapo watakaotoka wakifuata

mafundisho ya uongo wanapodanganywa na kupumbazwa na ahadi za uongo ambazo hawawezi kupata. Pili, kulikuwako wapinga Kristo wengi walioishi wakati Yohana alipokuwa akiandika maneno hayo, takribani miaka elfu mbili iliyopita. Hii inatofautiana na mafundisho yanayodai kwamba kuna “mpinga Kristo,” mmoja tu na kwamba ni mtu atakayejitokeza katika tukio lijalo. Mpinga Kristo ni mtu yeyote aliye kinyume na Kristo kwa njia yoyote ile. Mnyumbulisho wa maneno ni: “Mpinga” inamaanisha “kinyume,” na “Kristo,” inamaanisha “Kristo.” Kinyume na Kristo! Hata Waislamu ni wapinga Kristo kwa sababu wanakataa waziwazi kwamba Yesu ni Kristo kama ilivyo kwa wengine katika ulimwengu wa kidini. Toka Kristo alivyoishi, kuna wapinga Kristo wengi, na kwa huzuni, kutakuwa na wengi. Usiwe mmoja!

Alex Sadat Silvester











